# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**ALLIANCE GIRLS HIGH SCHOOL**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 3**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

# ALLIANCE GIRLS HIGH SCHOOL KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

**102/3**

**Karatasi ya 3**

**FASIHI**

**Mwongozo wa kusahihisha**

1. Ushairi
   (a) Anwani :Chema/ chema hakidumu/chema wangu.
   (b) Bahari
   Ukaraguni - kila ubeti una vina tofauti.
   Kikwamba - Neno 'chema ' limeanza beti zote.
   Utenzi - kila mshororo una mizani 12.
   Tarbia - Kila ubeti una mishororo mine.
   Mathnawi- sehemu mbili ukwapi na utao. *(Zozote 2 x 2 = 4)*
   (c ) Maudhui – <u>maombolezi</u> - Mshairi anaomboleza kwa kufiwa na wapenzi wake : mwanawe babaye (Kibwana Bashee) na nyanyake (Poni) *(Kutaja 1, kufafanua 1 = 2)*
   (d) (i) Tabdila - Kukingojeleza - kukingojelea
   Yakwe - yake

   (i) Kuboronga sarufi - Kipenzi nyanyagu - nyanyangu kipenzi

   (ii) Inkisari - Kinshariliza - kimeshaniliza/kimekwisha niliza
   n'ongeza - niongeza , haniambia - haniambii
   kinn'ondoka - kimeniondoka
   alojibu - aliyejipa
   (iv) Lahaja - ele -ila
   (e) Beti za mwisho mbili
   -Kila ubeti una mishororo minne
   -Kila ubeti una ukwapi na utao/vipande viwili/ mbili sehemu
   -Kila mshororo una mizani kumi na miwili; 6, 6
   -Vina vya ukwapi na utao ni tofauti (vinabadilika)
   -Maneno 'chema wangu' ndiyo yanayozianza beti hizi.
   -Kituo ni kimalizio tu. Kinabadilika. *(Zozote 4 x 1 = 4)*

(f) Tamathali - Takriri - neno chema
Balagha - mwanangu yu wapi?
ela kumzika? *(Kutaja ½ kufafanua ½ )*

(g) Msamiati
(i) Kitakuteleza - kitakutoka ghafla/kitakuponyoka.
(ii) Kinshaniliza - kimenifanya nilie

*(iii)* ela- isipokuwa bali *(3 x 1 = 3)*

**SEHEMU B: TAMTHILIA**

Timothy Arege: Mstahiki Meya

2. (a)
   (i) Msemaji ni Siki/Daktari Siki

(ii) Msemewa ni Tatu - mmoja wa wa wakilishi wa wafanyikazi
(iii) Mahali: Katika Ofisi ya daktari Siki
(iv) Sababu: Tatu amekuja kumwomba/kumsihi Daktari Siki aende aseme na Meya kama binamu yake,pengine huenda akamsikiliza. *(Hoja 4 x 1 = 4)*

(b) Tamathali za lugha:
(i) Msemo - Msikate tama
(ii) Tashihishi - Mlango huenda ukasalimu amri *(Hoja 2 x 2 = 4)*

(c) (i) Mishahara duni, kulipwa nusu/kukosekana hata baada ya miezi mitatu

(ii) Kuvunjiliwa mbali kwa maandamano ya wafanyi kazi

(iii) Kukosekana kwa dawa hospitalini

(iv) Madiwani kuongezwa mishahara

(v) Madiwani kutolipa kodi

(vi) Ufisadi – unyakuzi wa ardhi, kuuza fimbo ya Meya

(vii) Kukosekana kwa ajira kwa vijana

(viii) Hali duni ya usafi wa mazingira

(ix) Vifo vya watu hospitalini.

*(x)* Njaa – mtoto kulishwa kiporo *(Hoja zozote 7 x 2 = 14)*

3. Maudhui ya kutowajibika katika Kidagaa Kimemwozea.
- Meya kulinganisha ufanisi wa eneo na wa miji midogo na dhaifu, badala ya kuendelea kupiga hatua mbele wanapiga hatua kinyumenyume.
- Meya kujifanya hajui watu wanateseka. Amefumba macho kwa matatizo.

- Meya kukataa kuonana na kuwasikiza viongozi wa wafanyikazi, hata anapokutana nao anapuuza mapendekezo yao.

- Kuna baadhi ya watu wanaomuunga Meya mkono, hataki kujua juu ya wengi. Wachache wanatosha.

- Nyimbo za kizalendo baada ya na kabla ya vipindi muhimu, miaka hamsini baada ya uhuru.

- Mipango ya miaka kumi inapuuzwa. Meya anasema kuwa wana mipango ya milenia. Mipango ya miaka kumi ni upuzi.

- Afya bora na ya bure ilihaidiwa wananchi, wanalazimika kulipa.

- Wananchi kutoshirikishwa katika maamuzi. Wengine kama Siki kutimuliwa nyumbani mwa Meya, wanapojaribu kumweleza matatizo ya raia.

- Mikutano nadra kufanywa kama tunavyoelezewa na Diwani I – hufanywa hasa wakati kuna jambo kama mgomo kutokea.

- A hadi za uongo- shehena ya dawa kuwa bahari kuu.

- Kazi ya baraza/madiwani – badala ya kusikiza na kuwatimizia haja, wanafanya maisha ya wanacheneo kuwa mgumu zaidi.

- Uchafu kuenea kila mahali na uvundo kutokeza hata ndani ya majumba.

- Meya kukataa kuongea na wanahabari na wanchi kwa kusingizia kuwa ana wageni.

- Askari kuwafurusha watu kutoka mjini.Mji kubaki mahame

- Viongozi/madiwani wana njaa na tamaa kubwa isiyoweza kushibishwa.

- Washauri wanawatenga wengine. Diwani III anapuuzwa na wengine.

- Kujiongeza mishaharaa kama overtime marupurupu na kadhalika.

- Kula viapo vya kuficha siri za wizi kama wa fimbo ya meya.
- Meya kutojua kuwa hakuna maji safi. *(Zozote 10 x 2 = 20)*

**SEHEMU C: RIWAYA**

4. Kidagaa Kimemwozea

a) Mbinu za kifasihi katika dondoo
  - Tashbihi – Wawaone kama abiria wenzao.
  - Istiari – Mashua ( Ndoa inalinganishwa na mashua).

b) Jinsi msemaji hakustahiwa na mumewe

Msemaji ni Bi. Zuhura. Mumewe, Mtemi Nasaba Bora

  - Mtemi alimwacha Zuhura katika upweke alipojishughulisha na wanawake wengine kule njee k.m. Lowela.
  - Mtemi hakumruhusu Zuhura amwulize alikotoka. Alijia ukali ndipo asisemezwe.
  - Alimpiga (ushahidi ni kioo cha shubaka kilichokua na nyufa tele, tokeo la mapambano makali usiku mmoja baina yao.

- Mtemi alimtuhumu Zuhura kuwa na uhusiano na Amani alipowafumania katika chumba chake cha kulala.
- Mtemi alimtaliki Zuhura kwa tuhuma hizo.
- Mtemi alimzuia Zuhura kukinywesha kitoto Uhuru maziwa kilipopelekwa kwake na Amani baada ya kukiokota mlangoni pake.
- Zuhura hakutimiziwa haki yake katika ndoa kwani Mtemi aliporejea alijibwaga kitandani kama gogo la mti. (hoja 3x2= 6)

c) Maudhui inayojitokeza katika maneno ya Zuhura.

- Ukandamizaji wa jinsia ya kike. (2x1=2)

d) Mifano mingine ya ukandamizaji

- Dora hakusaidiwa na majisifu kuwalea watoto wao walemavu. Aidha, upo wakati majisifu alimtenga kwa miaka kumi na tano alipowazaa watoto wao wa kwanza wenye akili taahira.
- Mama mja mzito aliye kua akijifungua kando ya barabara hakupata usaidizi kutoka kwa Mtemi na Nasaba Bora.
- Lowela alilazimishwa na Mtemi kukitelekeza kitoto alichozaa kwa kukiwacha mlangoni kwa Amani.
- Mamake imani alinyanganywa shamba na nyumba yake kuchomwa na askari waliotumwa na Mtemi kwa maana alikua mjane.
- Bi kize alishurutishwa kuhudhuria mkutano wa siku kuu ya wazalendo, japo hakuelewa hotuba za Kiingereza alizosoma Mtemi.
- Imani alitupwa katika seli moja na Matuko Weye (wazimu) pamoja na Amani – askari hawakujali jinsia yake.
- Msichana mwanafunzi aliyeringwa na Fao baada ya kumtunga mimba.

5. Matumizi ya kweli kinzani katika kidagaa kimemwozea (al.20)

- Maana yake ni kinyume cha matarajioau kinaya.
- Mtemi Nasaba bora, maana yake ukoo bora au uungwana. Lakini vitendo vyake ni kinyume na jina lake hivyo ni kinaya. K.m
- Mtemi Nasaba bora aliwaadhibu wananchi ambao hawakuchanja mbwa wao ilihali wake mwenyewe hakuwachanja.
- Mtemi alimuuliza Amani ikiwa yeye ni mwizi wakati wa kutafuta ajira kwake ilihali yeye menyewe ndiye mwizi mkubwa aliyenyakua mali ya watu.
- Mtemi Nasaba bora alikuwa na tabia mbaya zisizo na ungwana wowote.
- Mtemi anapomwambia Amani kachukue “mwanao” akamtunze (akimrejelea motto uhuru ) ni kinaya kwa sababu Uhuru hakuwa mwana wa Amani bali wa Nasaba Bora.
- Mtemi kutumia lugha ya kizungu ambayo wananci wengi hawaelewi ni kinaya badala ya kutumia lugha ya Kiswahili wanayojua.
- Tabia za Nasaba Bora na mwalimu majisifu zilkua kinyume cha maadili ya kasisi baba yao. (yeye aliwataka wapendane na kusoma bibilia) ni kinaya maana hawakupendana hata kidogo wala hawakuwa wakisoma bibilia.
- Zahanati ya nasaba bora ina jina lenye maana ya utu lakini watu wengi huenda kufa huko.
- Ni kinaya kuona kuwa mtemi Nasaba nora alikuwa akisoma bibilia lakini anapoambiwa kuwa Bob Dj alikuwa ameumwa na jibwa “jimmy” alikataa kutoa usaidizi wa kumfikisha kwa matibabu akisema hayo ni stahili yako.

- Katika hotuba ya siku kuu ya wazalendo, mtemi anasema wanajali maslahi ya kila mmoja ilhali wananyanyasa watu na hawajali maslahi yao.
- N kinaya kuwa watu wa sokkomoko walikuwa na uchechefu wa maji ilhali kulikuwa na maji mengi katika mto kiberenge. Walibadilisha mtazamo wao kuhusu mwiko wa kutumia maji yam to huo wakati Imani na Amani walipokunywa maji bila kufariki.

- ni kinaya mwalimu majisifu kuitikia mwaliko wa chuo kikuu cha mkokotoni ilhali hakuwa na ufahamu wa mada ya kuwasilisha.
- Chwechwe Makwece aliletea nchi yake sifa nyingi lakini alipovunjika mguu hakusaidiwa, mguu ukakatwa.
- Watu wa tomoko walipigania uhuru lakini viongozi walioshika hatamu ndio waliofaidika zaidina kuwangandamiza kama mkoloni mzungu.
- Mwalimu majisifu alihojiwa katika idhaa ya taifa ya Tomoko (ITT) kuhusu maswala ya haki, uzalendo na utamaduni. Alitarajiwa kuwa miongoni mwa watetezi aalimu na staid wa utamaduni na uzalendo wa mwafrika lakini tunaona hatimaye majisifu mtu aliyekolea katika ulevi kama pale kwa mama n'tilie.
- Mwalimu majisifu alimpa nasaha mashaka kuwa wasome kwa bidii kwani bara Afrika ilitaka watu waliosoma sana ili kulikomboa toka kwenye utumwa na ujinga, njaa na umaskini ilhali yeye mwenyewe alifika darasani kufunza kwa nadra. (Hoja zozote 10x2=20)

**<u>SEHEMU YA D</u>**

**HADITHI FUPI – KEN WALIBORA, DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE**

**Mke Wangu**

6. (a) (i) Maelezo ya msimulizi
(ii) Anajiambia nafsini mwake/anaongea na nafsi yake

(iii) Mahali ni kwa kina msimulizi nyumbani

*(iv)* Alitaka kumwoa mke ambaye hakuwa amejifunza mengi ya mijini. Yule mshamba ambaye ni yeye/ndiye angamfundisha *(Hoja 4 x 1 = 4)*

*(b)* Alitaka mwanamke ambaye hajaathirika na maisha mjini na ambaye hangemsumbua bali yule ambaye yeye mwenyeww angemwelekeza jinsi anavyopenda. (*Hoja 1 x 2 = 2)*

(c) Migogoro baina ya msemaji – msimulizi na mwanamke huyu- Aziza:

-Aziza ana mtazamo wa kihafidhina kutokana na malezi yake ya shamba ilhali mumewe ana mtazamo wa kisasa unaoendana na maisha ya mjini pamoja na elimu aliyopata.

-Msimulizi anadhani akioa mwanamke wa shamba ataweza kumwelekeza jinsi anavyotaka yeye lakini anashindwa k.m

- Amekataa kuvaa viatu,
- Amekataa kusugua meno kwa mswaki na dawa
- Mkono wake umeparara n.k

-Aziza haoni sababu ya mumewe. Kuzidi kuwategemea wazazi kwa mahitaji yao ya kila siku, wao ndio wamlishe mumuwe na Aziza

-Aziza hafurahishwi na mtindo wa mumewe baada ya kumaliza masomo,kukosa kazi ya ofisi , ameketi bila kufanya chochote.

-Ubaguzi unaonyeshwa na mumewe wa walio wa tabaka la chini haumfurahishi Aziza ndiposa anamwalika bazazi wa madafu ghorofani.

-Aziza hapendi kukaa tu na kuletewa chakula,kuoshewa nguo na watumishi wa nyumbani bali kuyatekeleza haya mwenyewe. *(Hoja 6 x 2 = 12)*

**Damu Nyeusi**

7. Mifano kuoyesha mzungu hampendi mwafrika
   -Gari la mzungu halimbebi mwafrika.
   -Dereva mzungu halisimamishi gari kwa fikirini – anawashukiwa kuwa jambazi
   -(ii) Akiwa darasani, Fikirini anaulizwa maswali ya kumdhalilisha na kumdunisha k.m
   -Kwenye uwanja wa ndege hapa Marekani
   -Mikahawani, Fikirini aliangaliwa na macho meupe yenye dharau ya wateja wazungu.
   -Fikirini kushtakiwa mahakamani eti hakufunga zipu.
   -Mwanamke yule mweusi kwa ushirikiano na jibaba, wanamfungia ndani kumlazimisha Kimapenzi.
   -Alitishwa maisha yake kwa mtutu wa bunduki na yule jibaba.
   -Dada mweusi anamwelekea kisu chenye makali ubavuni
   -Fikirini alidhalilishwa kwa kuvuliwa nguo zote.
   -Fikirini alinyang'anywa mali yake yote vikiwemo vitabu
   -Fikirini anatusiwa – tumbiri
   -Fikirini anatozwa faini mara mbili na polisi mzungu kwa kuvuka barabara huku taa kuelekea magari zikiwa zimewaka rangi nyekundu – wazungu wanaachwa kupita tu.
   -Wahadhiri wanatoa alama kwa kupendelea watu weupe na kuwakandamiza weusi.
   -Fikirini akienda kununua vitu kwenye duka mlinzi humfuata kwa kushukiwa wizi.

   *(Hoja zozote 10 x 2 = 20)*

8. (a) Sifa za ngomezi
   -Huwasilisha ujumbe mzito kwa njia iliyofichika kwa mapigo ya ngoma
   -Wanajamii wa kundi husika huweza kufasiri ujumbe
   -Inatumiwa kutangaza jambo fulani
   -Inapatikana kwa wingi katikajamii mbalimbali za kiafrika
   -Hupiga marufuku katika eneo la kutolea kafara
   -Ngoma hutumiwa kunawasilisha ujumbe wa aina yoyote.(5x 1 = 5)

(b) Sifa za miviga
   -Huwa na madhumuni maalum ya kufanya sherehe hizo
   -Huwa na wakati maalum wa kuitekeleza
   -Kuna utaratibu maalum wa kufanya sherehe hiyo
   -Kuna sheria/kaida maalum zinazozingatiwa wakati wa shule hizo
   -Hujumuisha vitendo maalum – km kusimama
   -Aghalabu hutolewa sadaka za vitu mazaao au wanyama
   -Huwa na matumizi ya vifaa maalum na mavazi (maleba)
   -Hufanywa kwa lugha maalum inayofungamana na sherehe (Mivigi mingine hufanywa kimyakimya bila maneno) *(5 x 1 = 5)*

(c) Hasara za miviga *(5 x 2 = 10)*
   -Baadhi ya miviga huhatarisha maisha na afya ya wanajamii kama vile kumrithi mjane,jando-vifaa butu.
   -Hukinza malengo ya kitaifa-ukeketaji wa wanawake.
   -Huhusisha ushirikina unaozua uhasama baina ya watu-mazishi.
   -Hugharimu pesa nyigi na kuiacha familia katika hali duni kiuchumi.
   -Husababisha uchungu –ukeketaji au jando.
   -Huendeleza tofauti za kijinsia-unyago na jando-humdhalilisha mke na kumtukuza mume.
   -Huasi mabadiliko ya kiwakati-zimepitwa na wakati.

– Zozote 4 x 1 = 4